**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI**

# TAARIFA KWA UMMA

## KUHUSU MAELEKEZO YA KISERA

Kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 4, 19(3), 14(2), 84(3)(a) na (b) na 164 vya Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya Mwaka 2024, na kifungu cha 26 cha Sheria ya Tume Huru ya Uchaguzi Na. 2 ya mwaka 2024, Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi inatoa **MAELEKEZO YA KISERA KATIKA UCHAGUZI MKUU WA MWAKA 2025** kama ifuatavyo:-

1. kwa mpiga kura asiye na picha katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura lakini ana kadi ya Mpiga Kura yenye taarifa binafsi zilizomo katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura, **ARUHUSIWE KUPIGA KURA;**

2. kwa mpiga kura ambaye ana kadi yenye namba ya mpiga kura inayotofautiana na namba ya mpiga kura iliyomo katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura lakini taarifa nyingine zote ikiwemo picha na majina yaliyopo katika Daftari la Kudumu la Wapiga kura ni sawa kama ilivyo katika kadi ya mpiga aliyonayo; **ARUHUSIWE KUPIGA KURA;**

3. kwa mpiga kura ambaye ameandikishwa katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura na taarifa zake zipo katika Daftari la Kudumu la Wapika Kura lililopo katika kituo husika, lakini amepoteza kadi yake au kadi yake imeharibika, **ARUHUSIWE KUPIGA KURA** kwa kutumia mojawapo ya vitambulisho vifuatavyo:



UCHAGUZI MKUU OKTOBA 29, 2025
Kura Yako Haki Yako Jitokeze Kupiga Kura

i. Kitambulisho cha Taifa (NIDA);

ii. Leseni ya udereva; au

iii. Pasi ya kusafiria(*Passport*)

Lakini kwa sharti kwamba, majina yake yaliyopo katika kitambulisho atakachowasilisha mpiga kura, ni lazima yafanane na majina yote kama yalivyo katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura.

4. kwa mpiga kura ambaye ana kadi ya kupigia kura lakini taarifa zake hazipo katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura **ASIRUHUSIWE KUPIGA KURA**; na

5. kwa wapiga kura wote kutoka katika kata 10 zilizofutwa ambazo ni Kata ya Kanoge, Litapunga, Katumba, Mtapenda (Kijiji cha Ikolongo na Ndurumo) vilivyopo katika Jimbo la Nsimbo Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo, Kata ya Mishamo, Ilangu, Bulamata na Ipwaga zilizopo katika Jimbo la Tanganyika Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika na Kata ya Milambo, Igombemkulu na Kanindo zilizopo katika Jimbo la Ulyankulu Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua ambazo wapiga kura walihamishiwa katika kata za jirani lakini kadi zao zinaendelea kusoma taarifa za awali za vituo vyao vya zamani vilivyofutwa, **WARUHUSIWE KUPIGA KURA KATIKA VITUO VIPYA WALIVYOHAMISHIWA.**

Imetolewa leo siku ya Alhamis tarehe 23 Oktoba, 2025; na

Kailima, R. K

**MKURUGENZI WA UCHAGUZI**

UCHAGUZI MKUU OKTOBA 29, 2025
Kura Yako Haki Yako Jitokeze Kupiga Kura